TANGAZO LA SERIKALI NA. 950 la tarehe 29/11/2019

SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA NA. 272)

———

AMRI

———

(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 219(1) (d))

AMRI LA MAREKEBISHO YA BEI YA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA MUGANGO-KIABAKARI (MUGANGO-KIABAKARI WSSA), 2019

Utangulizi

1.Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugango-Kiabakari(Mugango-KiabakariWSSA), (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Maji safi na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2019.

Tarehe ya kuanza kutumika

2. Amri hii itachukuliwa imeaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Disemba, 2019.

Marekebisho ya bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Mugango-KiabakariWSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Amri hii.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

(a) ifikapo tarehe 31 Disemba, 2019 au kabla, Mugango-KiabakariWSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya AMRI hii;

(b) Mugango-Kiabakari WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la AMRI hii;

(c) Mugango-KiabakariWSSA itafikia viashiria

vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la AMRI hii;

(d) Mugango-Kiabakari WSSA itawekeza katika kudhibiti upotevu wa maji kutoka 84.6% kwa sasa hadi 40% kwa mwaka 2021/22 kwa kubadilisha km 0.4 mwaka 2019/20; km 2 mwaka 2020/21; na km 2.9 kwa 2021/22;

(e) ifikapo au kabla ya tarehe 31 Disemba 2019 Mugango-Kiabakari WSSA itaacha kuhamishia dira za wateja kutoka majumbani kwenda kwenye bomba kuu la kusambazia maji;

(f) Mugango-Kiabakari WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Amri ya Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yalivyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne;

(g) Mugango-Kiabakari WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Mugango-Kiabakari WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Mugango-Kiabakari WSSA katika siku zijazo;

(h) Kuanzia tarehe 1 Septemba 2019, Mugango-Kiabakari WSSA itaanza kulipa tozo ya EWURA kwa mujibu wa kifungu namba 43 cha Sheria ya EWURA, Sura 414 na kifungu namba 6 cha Kanuni za EWURA kuhusu

Taratibu za Kukusanya ada na tozo zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali namba193 la mwaka 2010;

(i) Ifikapo tarehe 30 Septemba, 2019, au kabla, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugango-Kiabakari itatakiwa iwasilishe EWURA vielelezo kwamba ilitoa taarifa kwa Wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma kuhusu utekelezaj wa bei mpya, ikiwa pamoja na wawakilishi wa wanachi, Serikali na viongozi wa dini katika eneo lake la huduma.

Amri Na. 11-014 la tarehe 1 Juni 2011

5. Amri hili linasitisha matumizi ya AMRI Na. 11-014 la tarehe 1 Juni 2011 katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mugango-Kiabakari (Mugango-Kiabakari WSSA).

———

MAJEDWALI

———

JEDWALI LA KWANZA:

———

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

———

(Imetengenezwa chini ya aya ya 3)

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	BeizaSasa	BeiZilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	345	1,100	1,200	1,300
Taasisi	335	1,110	1,300	1,400
Biashara	510	1,640	1,910	1,970
Magati	1000	1,000	1,000	1,000
Viwandani	0	1,640	1,910	1,970
Wastani	407	1,310	1,520	1,570

Jedwali Namba 1(b): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho ya Maji Safi (Shilingi/Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada yaSasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	30,000	Asilimia 20 yagharamazavifaanaufundikamailivyobainish wakatikaKanunizaMajisafizamwaka 2013		
Taasisi				
Biashara				

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

Kundi la Wateja	Ada yaSasa	Ada Zilizoidhinishwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	5,500	15,000	15,750	16,540
Taasisi	11,000	20,000	20,000	20,000

Biashara	11,000	20,000	20,000	20,000
Magati	11,000	20,000	20,000	20,000

———

JEDWALI LA PILI

———

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA(Shilingi Milioni)
(Imetengenezwa chini ya aya ya 4(b))

Maelezo ya kazi/vifaa			
	2019/20	2020/21	2021/22
Ukarabati na ubadilishaji			
Manunuzi ya dira za maji, dira 30 kwa mwaka 2019/2020, dira 60 kwa maka 2020/21 dira 60 kwa mwaka 2021/22 kwa ubadilishaji	2.49	4.15	4.15
Ukarabati na ubadilishaji wa bomba kuu la kusafirishia maji kilomita 0.4 kwa mwaka2019/20, kilomita 2 kwa mwaka 2020/21 na kilomita 2.9 kwa mwaka 2021/22 .	80.00	400.00	580.00
Jumla ndogo(Ukarabati na ubadilishaji)	82.49	404.15	584.15
Uwekezaji mpya			
Manunuzi ya dira za maji 285 kwa mwaka 2019/2020, dira 232 kwa mwaka 2020/21 na dira 724 kwa mwaka 2021/22 kwa Maunganisho mapya	17.71	21.99	60.09
Manunuzi ya dira za maji za malipo kabla (LIMAKU), dira 15 pamoja mfumo wake wa kompyuta kwa mwaka 2020/21 and dira 15 kwa mwaka 2021/22	0.00	17.25	11.25
Manununzi ya dira kubwa za maji za usambazaji, dira 6 kwa mwaka 2020/21 maeneo ya Mugango kati, kijiji cha Ryamugabo, Butiama, Kiabakari-Butiama na mtaa wa Madara dira 1 kwa kijiji cha Bisarye	0.00	6.18	0.84

Tangazo la Serikali Na. 950 (Linaendelea.)

Maelezo ya kazi/vifaa			
	2019/20	2020/21	2021/22
Upanuzi wa mtandao wa usambazaji maji (Bomba la kipenyo cha 63milimita na 50milimita , daraja C. kilomita 22 kwa mwaka 2020/21, kilomita 28 kwa mwaka 2021/22) maeneo ya Kurwaki, Singu Mahakani, Makole, Buturu, Busaraga,Kukiyugu, Muryaza and Mwanzaburiga	0.00	213.73	268.97
Manunuzi ya pikipiki 1 kwa mwaka 2020/21 na pikipiki 1 kwa mwaka 2021/22	0.00	1.50	1.56
Manunuzi ya kompyuta 1 kwa mwaka 2019/2020, kompyuta 2 kwa mwaka 2020/21 na kopmyuta 2 kwa mwaka 2021/22	2.00	2.08	2.17
Manunuzi ya Printa 1 kwa mwaka 2019/20 na mashine ya kopi 1 kwa mwaka 2020/21	0.50	2.00	0.00
Jumla Ndogo(gharama za uwekezaji mpya)	20	265	345
Jumla Kuu ya Gharama za Uwekezaji	103	669	929

———

JEDWALI LA TATU

———

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)
(Imetengenezwa chini ya aya ya 4(c))

Maelezo	Uniti	Lengo la Utendaji		
		2019/20	2020/21	2021/22
Idadi ya wateja wapya wa majisafi	Na	285	232	724
Kiwango cha upotevu wa maji	%	51	47	40
Wateja wenye dira	%	100	100	100
Kiwango cha ufanisi katik aukusanyaji wa mapato (bila madeni)	%	90	92	95

JEDWALI LA NNE

GHARAMA ZILIZOIDHINISHWA (Shilingi Milioni)
(Imetengenezwa chini ya aya ya 4(f))

Gharama	2019/20	2020/21	2021/22
Uzalishaji	376.26	379.03	381.94
Usamabazaji	104.35	119.09	128.82
Matengenezo	42.68	49.18	53.00
Watumishi	111.51	119.95	136.60
Utawala	87.12	111.06	121.36
Matangazo	2.27	2.37	2.46
Matukio	2.00	2.04	2.08
Bodi	0.00	0.00	0.00
Fedha	1.00	1.04	1.08
Jumla ya gharama za uendeshaji na matengenezo	727.19	783.77	827.35
Uchakavu	102.70	668.88	929.03
Faida ya Uwekezaji	0	0	0
Jumla ya mahitaji ya fedha	829.89	1,452.65	1,756.38
Kutoa mapato mengineyo	23.27	20.36	62.08
Jumla ya mahitaji ya fedha yanayotokana na mauzo ya maji	806.62	1,432.29	1,694.30

Dodoma
14 Novemba, 2019

NZINYANGWA E. MCHANY
Mkurugenzi Mkuu